

## **BAADA YA KIFO KUNA NINI TENA?**

KIMETOLEWA NA: ROD RUTHERFORD

Je, Umewahi kujiuliza kitu gani kitafuata mara baada ya kifo? Wengi wetu mara nyingi au wakati mwingine tumekuwa tukifikiri kuhusu swala hili. Lakini katika kitabu cha Agano Jipya habari kuhusu swala hili ambalo limechanganya watu wengi na linazungumzia ni nini kitatokea baada ya kifo. Habari hii ilizungumzwa na Yesu na ipo katika kitabu cha Luka 16:19-31.

Habari hiyo inazungumzia juu ya watu wawili. Mmoja alikuwa tajiri, na alipata kila alichohitaji. Na mwingine alitwa Lazaro yeye alipendelea kulala penye mlango wa yule tajiri na kuomba makombo yaliyobakia au yaliyoanguka katika meza ya tajiri.

Baadaye Lazaro alifariki, pia tajiri naye alifariki. Ni kama ilivyokuwa tofauti kubwa ya maisha yao ya hapa duniani ndivyo ilivyokuwa hata baada ya vifo vyao. Ibrahimu alikwenda sehemu ya peponi, lakini tajiri alikwenda sehemu ya mateso.

Kuna mambo mengi tunayoweza kujifunza kutokana na habari hii. Jambo mojawapo ni kwamba utajiri, mamlaka na starehe za hapa duniani zitapita. Tajiri alikuwa na hivyo vyote lakini bado baada ya mauti alikuwa sehemu ya mateso. Lakini Lazaro hakuwa na vitu hivyo hapa duniani, lakini baada ya kifo aliurithi uzima wa milele.

Jambo jingine ni kwamba ufahamu upo baada ya kifo. Watu wengi wanafikiri hakuna ufahamu mpaka siku ya mwisho ambayo ni ya ufufuo, hii sio kweli. Mwili hulala kaburini lakini baada ya kifo. Tunaona kwamba baada ya kifo tajiri aliweza kumkumbuka Lazaro, pia alikumbuka kuwa alikuwa na nduguze watano duniani, aliwaonea huruma hata akamwomba ibrahimu atume watu waje wahubiri injili kwao ili wasije wakaja katika sehemu mbaya aliyokuwa.

Wazazi wengi baada ya kifo watawakumbuka watoto wao, hasa kwa jinsi walivyoshindwa kuwafundisha kuhusu mungu, ambapo walikuwa na nafasi ya kufanya hivyo. Wataomba mtu atumwe kuwafundisha ili nao wasije wakaja kwenye sehemu ya mateso ambayo wao wapo. Wengine watajuta wakikumbuka nafasi nzuri walizokuwa nazo hapa duniani ya kutubu, lakini haitasaidia.

Yesu katufundisha vile vile kufuatana na habari hii baada ya kifo hakuna nafasi tena. Tunaona tajiri aliomba angalau Lazaro achovye kidole kwenye maji na apoze ulimi wa tajiri, lakini Ibrahimu alikataa, na alisema kati yetu kuna shimo kubwa mtu hawezi kuvuka hapo. Mungu ametupatia nafasi ya kutubu tukiwa hapa duniani, **“Bwana hakawii kutimiza ahadi yake wafikirie toba,”** (2 Pet. 3:9). Kuna sehemu mbili tu za kwenda baada ya kifo. Kuna sehemu ya baraka ambayo lazaro alikwenda, hii ni sehemu ambayo wana wa Mungu waaminifu wanakwenda wakingojea ufufuo na hukumu. Pia kuna sehemu ya mateso ambayo tajiri alikwenda, sehemu hii huenda wale wote ambao hawakumwamini Mungu wakati walipokuwa hapa duniani.

Vipi mwenzangu? Umejitayarishaje kwa ajili ya kifo? Maisha ya hapa duniani hayana uhakika kwamba tutaishi na kuiona kesho. Kifo huja ghafla Biblia inatuonya **“Haya basi, ninyi msemao, leo au kesho tutaingia mji fulani na kukaa humo mwaka mzima, na kufanya biashara na kupata faida; walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, na kisha hutoweka,”** Yak. 4:13-14. Biblia tena inasema, **“Kwa maana asema wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa,”** 2 Kor. 6:2. Anza leo, wakati kuna nafasi, mwamini Yesu Kristo Mwana wa Mungu, Yoh. 8:24. Yeye ni njia ya kweli na uzima, Yoh. 14:6. Kwa jina la Yesu Kristo pekee ndilo tunaloweza kuokolewa kwalo, Mdo. 4:11-12. Tubu dhambi zako zote, Mdo. 17:30-31. Mkiri Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, Mdo. 8:37. Uzikwe pamoja naye katika ili upate ondoleo la dhambi, Rum. 6:4; Mdo. 22:16. Kisha mtumikie Kristo katika Kanisa lake kwa maisha yako yote yaliyosalia na utabarikiwa.

**“Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa nami nitakupa taji ya uzima,”** Ufu.2:10. **“Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake,”** 2 Tim.4:8.

[www.kanisalakristo.com](http://www.kanisalakristo.com)